TANGAZO LA SERIKALI Na. 224 la tarehe 29/3/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153 (1) (b))*

SHERIA NDOGO YA KUZUIA NA KUDHIBITI SUMUKUVU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI YA MWAKA 2024.

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Kuzuia na kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Bahi;

"kanuni bora za kilimo" maana yake ni uandaaji wa shamba kwa usahihi, upandaji mbegu bora kwa wakati na kwa nafasi sahihi, upaliliaji, utumiaji mbolea kwa usahihi, udhibiti wa wadudu na wanyama waharibifu, uvunaji na hifadhi sahihi wa mazao;

"kilimo" maana yake ni shughuli ya uzalishaji wa mazao;

"kuvu'' maana yake ni ukungu unaoota kwenye mazao;

"mkulima" maana yake ni mtu, taasisi, kampuni au kikundi cha watu kinachojihusisha na shughuli za kilimo;

"mfanyabiashara'' maana yake ni taasisi, kampuni, kikundi cha watu au mtu binafsi anayejihusisha na shughuli za kuuza au kununua mazao ya kilimo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mazao'' maana yake ni punje zinazotokana na mmea wa mhindi, mpunga, uwele, mtama, karanga, ngano, ufuta, alizeti, shayiri, ulezi na mazao ya mizizi yatokanayo na mihogo au viazi;

"sumukuvu" maana yake ni sumu inayozalishwa na kuvu wanaoota kwenye mazao;

"uhifadhi" maana yake ni utaratibu wa kutunza mazao katika sehemu ambayo haisababishi mazingira ya uotaji wa kuvu;

"ukaushaji" maana yake ni taratibu sahihi za kupunguza unyevu kwenye mazao kwa ajili ya matumizi au uhifadhi;

"usindikaji" maana yake ni hatua ya uchakataji wa zao kwa lengo la kuongeza thamani;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"uvunaji" maana yake ni uondoaji wa mazao kutoka kwenye mmea baada ya kukomaa au kukauka;

"viashiria vya sumukuvu" maana yake ni dalili zinazoonesha uwepo wa sumukuvu kwenye mazao ya mahindi, mpunga, uwele, mtama, karanga, ngano, ufuta, alizeti, shayiri, ulezi zilizovunjika, na mazao ambayo hayajauka vizuri;

"viuatilifu" maana yake ni sumu ya kuua au kuzuia wadudu waharibifu wa mazao;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za kilimo na Udhibiti wa Sumukuvu

**4**.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuratibu na kusimamia shughuli za kilimo ndani ya eneo la Halmashauri kwa lengo la kuzuia na kudhibiti sumukuvu.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kufanya ukaguzi katika mashamba, vyombo vya usafirishaji wa mazao, maghala,

kiwanda au eneo la usindikaji kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Uandaaji wa shamba

**5**. Mtu anayekusudia kulima, atapaswa kuzingatia misingi ifuatayo:
(a) kufuata njia sahihi za uandaaji wa shamba;
(b) kutayarisha shamba kwa wakati; na
(c) kutochoma moto.

Upandaji wa mazao.

**6**. Mtu atakayepanda mazao atapaswa kuzingatia njia sahihi za upandaji ikiwa ni pamoja na-
(a) kutumia mbegu bora;
(b) kupanda mazao mara tu mvua za kupandia zinapoanza kunyesha; na
(c) kupanda kwa nafasi sahihi.

Utunzaji wa mazao shambani

**7**. Mtu aliyepanda mazao atapaswa kuyatunza kwa kuzingatia njia sahihi za utunzaji wa mazao ikiwa ni pamoja na-
(a) kutumia mbolea;
(b) kupalilia kwa wakati; na
(c) kudhibiti magonjwa, wadudu au wanyama waharibifu.

Uvunaji wa mazao

**8**. Mtu yeyote atakayevuna mazao atapaswa kuvuna kwa kuzingatia kanuni bora za uvunaji ikiwa ni pamoja na-
(a) kuvuna mara baada ya mazao kukomaa au kukauka;
(b) kusafirisha na kuhifadhi vizuri; na
(c) kusafisha shamba baada ya kuvuna.

Ukaushaji wa mazao

**9**. Mtu atakayevuna mazao anapaswa kuyakausha kwa kutumia njia sahihi mara tu baada ya kuvuna ikiwa ni pamoja na:
(a) njia za asili zisizoruhusu kuvu kuota;
(a) kutumia maturubai, mikeka na vichanja vinavyozuia uchafuzi wa mazao; na
(b) kukausha kwa njia yoyote sahihi itakayoelekezwa na mtaalamu.

Uhifadhi wa mazao

**10**.-(1) Mtu atawajibika kuhifadhi mazao kwa kutumia njia sahihi za kiasili au za kisasa ambazo zitazuia kuota kwa kuvu.

(2) Njia sahihi zinazoelekezwa kutumika kuhifadhi mazao ni pamoja na-

(a) mifuko isiyopitisha hewa;
(b) magunia ya kawaida kwa ajili ya mazao yaliyowekwa viuatilifu;
(c) kihenge na kichanja bora cha asili;
(d) silo au pipa maalumu;
(e) ghala bora lililo safi;
(f) kutumia viuatilifu kwenye mazao kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu; au
(g) njia nyingine kadri itakavyoshauriwa na wataalamu.

Wajibu wa Halmashauri

**11**. Katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hii, Halmashauri itakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuhamasisha na kutoa elimu ya uzalishaji na usimamizi wa mazao;
(b) kuhamasisha uhifadhi wa mazao katika eneo au mahala salama ili kuepuka uchafuzi wa sumukuvu;
(c) kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo;
(d) kutunza kumbukumbu za mashamba yote ya mazao ya kilimo katika kata na vijiji ili kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;
(e) kuanzisha na kuendeleza mashamba darasa na vituo maalumu kwa ajili ya kutoa mafunzo ya udhibiti wa sumukuvu;
(f) kuanzisha na kuhamasisha wakulima na wadau wengine kujenga sehemu za kuhifadhi mazao; na
(g) kuandaa uwepo wa vituo maalumu vya kuuza na kununua mazao.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kumteua Afisa Mwidhiniwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

**12**. Kila mkulima atakuwa na wajibu ufuatao:

Wajibu wa mkulima

(a) kufanya shughuli za kilimo kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo na usimamizi wa mazao kabla na baada ya kuvuna;
(b) kutoa taarifa kwa Halmashauri kuhusu uwepo wa dalili za kuvu katika mazao; na
(c) kushiriki mafunzo yaliyoandaliwa na Halmashauri ya kudhibiti sumukuvu na kutekeleza ujuzi uliopatikana kwenye mafunzo hayo.

Wajibu wa msafirishaji

**13**. Mtu anayesafirisha mazao anapaswa kuhakikisha vifungashio na vifaa anavyotumia kusafirisha mazao ni vikavu au visivyoruhusu maji, unyevu na vumbi kuingia ndani ili kuepusha kuvu kuota kwenye mazao.

Wajibu wa mfanyabiashara

**14**. Kila mfanyabiashara wa mazao atakuwa na wajibu wa kuhakikisha ananunua, anahifadhi, anasafirisha au kuuza mazao ambayo hayana viashiria vya uwepo wa sumukuvu kama vilivyoanishwa katika Jedwali la Kwanza.

Wajibu wa msindikaji

**15**. Kila msindikaji atakuwa na wajibu wa kusindika mazao ambayo hayana viashiria vya uwepo wa sumukuvu kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Makosa na adhabu

**16**. Mtu ambaye-
(i) hataandaa, hatapanda au kutunza shamba na mazao kwa usahihi;
(ii) hatavuna kwa wakati mara baada ya mazao kukomaa;
(iii) atachelewa kuondoa mazao shambani baada ya kuvuna;
(iv) ataanika mazao kwenye udongo, vumbi au mchanga;
(v) atakausha mazao katika mazingira yanayoweza kusababisha sumukuvu;
(vi) atatumia viuatilifu vilivyozuiliwa kutumika kwenye mazao;
(vii) atauza mazao yenye viashiria vya sumukuvu;

(viii) atasafirisha mazao kwa njia zitakazosababisha mazingira ya kuvu kuota;

(ix) atatumia mazao yenye viashiria vya sumukuvu wakati wa usindikaji; au

(x) atatenda jambo lolote lililokatazwa na Sheria Ndogo hii,

anatenda kosa na endapo atapatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi mbili au vyote kwa pamoja.

Ufifilishaji wa makosa

**17**. Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini endapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi katika fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 14 na 15)*

VIASHIRIA VYA SUMUKUVU

| Namba | AINA YA MAZAO | HALI YA UNYEVU AU KUVU | MWONEKANO WA PUNJE |
|---|---|---|---|
| 1 | Mahindi | Punje kuwa na unyevu | Punje kuwa na ukungu au kuvu - rangi kahawia au nyeusi au kijani au njano kuwa na harufu ya uvundo |
| 2 | Karanga | Punje kuwa na unyevu | Punje kuwa na ukungu au kuvu – rangi kahawia au nyeusi au kijani au njano kuwa na harufu ya uvundo |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 17)*

FOMU YA KUFIFILISHA MAKOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashuri ya Wilaya ya Bahi, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ya Mwaka 2024.

Na kwamba niko tayari kulipa kiasi cha shilingi ................................. kwa ajili ya kufifilisha kosa nililotenda.

Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo tarehe…………. ya mwezi…………..… mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU :
Jina:……………………………………..…………………….....
Saini……………………….…………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Bahi imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Mwadiwani la Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe 25/6/2022, mbele ya:-

Zaina mfaume mlawa,,
*Mkurugenzi mtendaji(W),*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bahi*

Donald simando mejitii,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bahi*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
30 Januari, 2024.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*